**KAULI YA TAARIFA YA CHANJO**

# Chanjo ya Ndui/Monkeypox (JYNNEOS™): *Unachohitaji Kujua*

Many Vaccine Information Statements are available in Swahili and other languages. See www.immunize.org/vis

Kauli nyingi za taarifa ya chanjo zinapatikana katika Kiswahili na lugha nyinginezo. Angalia www.immunize.org/vis

## 1. Kwa nini uchanjwe?

**Chanjo ya ndui/monkeypox (JYNNEOS™)** inaweza kusaidia kulinda dhidi ya ndui, monkeypox na magonjwa mengine yanayosababishwa na virusi vya orthopox, ikiwemo kirusi cha vaccinia.

Ndui ni ugonjwa mbaya sana unaosababishwa na kirusi cha variola. Baadhi ya watu huendelea kuwa katika hatari ya kutagusana na kirusi hicho kinachosababisha ndui, ikiwemo watu wanaofanya kazi katika hali za dharura na baadhi ya wafanyakazi wa maabara. Virusi hivi vinaweza kuenea kutoka kwa mtu mmoja hadi kwa mwingine, na kusababisha dalili ikiwemo joto jingi na upele. Watu wengi waliokuwa na ndui hapo awali walipona, lakini karibu watu 3 kati ya 10 walio na ugonjwa huo walikufa.

Monkeypox ni ugonjwa nadra wenye dalili ambazo zinafanana na ndui, lakini ambazo ni hafifu kuliko dalili za ndui. Hata hivyo, monkeypox inaweza kusababisha kifo. Monkeypox ni maambukizo yayojitokeza barani Afrika na milipuko ya visa vya monkeypox kutoka ng'ambo wakati mwingine hutokea katika nchi nyingine, ikiwemo Marekani.

Virusi vya vaccinia vinaweza kusababisha ugonjwa wakati watu wanatagusana na watu walioambukizwa (kama vile kugusana na mtu ambaye hivi karibuni alipata chanjo ya ACAM2000®, aina nyingine ya chanjo ya ndui) au wanyama. Watu wanaoshughulika na virusi vya vaccinia katika maabara wanaweza kugusana kwa bahati mbaya na virusi hivyo, na wakiambukizwa, wanaweza kuwa wagonjwa. Hata hivyo, maambukizo mengi ya virusi vya vaccinia huondoka yenyewe bila matibabu.

## 2. Chanjo ya ndui/monkeypox (JYNNEOS™)

Chanjo ya ndui/monkeypox (JYNNEOS™) inatengenezwa kwa kutumia kirusi hai cha vaccinia kilichodhoofishwa na haiwezi kusababisha ndui, monkeypox, au ugonjwa mwingine wowote wa kuambukiza.

JYNNEOS™ imeidhinishwa na Shirika la Chakula na Dawa (Food and Drug Administration - FDA) kwa ajili ya kuzuia ugonjwa wa ndui na monkeypox katika **watu wazima wenye umri wa miaka 18 au zaidi walio katika hatari kubwa ya kuambukizwa ndui au monkeypox**.

- Shirika la CDC linapendekeza JYNNEOS™ kwa wafanyakazi fulani wa maabara na wahudumu wa dharura ambao huenda wakagusana na virusi vinavyosababisha maambukizo ya virusi vya orthopox.
- CDC inapendekeza chanjo hii ifikiriwe kuchanjwa watu wanaotoa ACAM2000®, au wanaowauguza wagonjwa walioambukizwa virusi vya orthopox.

JYNNEOS™ kwa kawaida hutolewa kama mfululizo wa sindano 2, baada ya wiki 4. Watu ambao wamepokea chanjo ya ndui hapo awali wanaweza kuhitaji dozi 1 pekee.

Dozi za kiongeza nguvu zinapendekezwa kila miaka 2 au 10 ikiwa mtu anaendelea kuwa katika hatari ya kugusana na virusi vya ndui, monkeypox, au virusi vingine vya orthopox. Mtoa huduma wako wa afya anaweza kukupatia habari zaidi.

## 3. Zungumza na mtoa huduma wako wa afya

Mwambie mtoa huduma wako wa chanjo ikiwa mtu anayepokea chanjo:

- Amekuwa na **mmenyuko wa mzio baada ya dozi ya chanjo ya ndui ya hivi karibuni**, au ana **mizio yoyote mibaya inayotishia maisha**
- Ana **mfumo wa kinga uliodhoofika**
- Ni mjamzito au anafikiria ana **ujauzito** au **ananyonyesha**

Katika visa fulani, mtoa huduma wako wa afya anaweza kuamua kuahirisha uchanjaji wa kawaida (kabla ya mtagusano) wa ndui/monkeypox wa JYNNEOS™ hadi katika ziara ya hapo baadaye.

Watu walio na magonjwa madogomadogo, kama vile mafua, wanaweza kuchanjwa. Watu ambao ni wagonjwa kidogo au wagonjwa sana wanapaswa kwa kawaida kungojea hadi wapone kabla ya kupokea dozi ya kawaida (kabla ya mtagusano) ya JYNNEOS™. **Ikiwa imependekezwa upokee JYNNEOS™ kutokana na mtagusano na virusi vya monkeypox, unapaswa kuchanjwa pasipo kujali magonjwa ulionayo wakati huo, ujauzito, kunyonyesha, au mfumo dhaifu wa kinga.**

U.S. Department of Health and Human Services
Centers for Disease Control and Prevention

JYNNEOS™ inaweza kwa kawaida kutolewa pasipo kujali muda wa kutolewa kwa chanjo nyingine. Hata hivyo, watu fulani walio katika hatari zaidi ya kupata ugonjwa unaoitwa myocarditis (kuvimba kwa misuli ya moyo), ikiwemo wanaume vijana, wanaweza kuamua kungoja wiki 4 baada ya chanjo ya JYNNEOS™ kabla ya kupokea chanjo fulani za COVID-19. **Ikiwa imependekezwa upokee JYNNEOS™ kwa sababu ya mtagusano na virusi vya monkeypox, unapaswa kuchanjwa hata ikiwa hivi karibuni ulipokea chanjo ya COVID-19.**

## 4. Hatari za athari ya chanjo

- Wekundu, maumivu, kuvimba, na mwasho kwenye sehemu iliyodungwa sindano ndivyo vitu vya kawaida zaidi ambavyo hufanyika baada ya chanjo ya JYNNEOS™.
- Uchovu (kuchoka), maumivu ya kichwa, na maumivu ya misuli yanaweza pia wakati mwingine kutokea baada ya kuchanjwa JYNNEOS™.

Nyakati nyingine watu huzirai baada ya taratibu za kimatibabu, ikiwemo kuchanjwa. Mwambie mtoa huduma wako ikiwa unahisi kizunguzungu au mabadiliko katika kuona kwako au kuhisi milio masikioni.

Kama ilivyo na dawa yoyote, kuna uwezekano nadra sana kwa chanjo kusababisha mzio mbaya, majeraha mengine mabaya, au kifo.

Unaweza kujisajili katika V-safe baada ya kupokea dozi yoyote ya chanjo ya JYNNEOS™ kwa kutumia simu mahiri yako na kwenda kwenye **vsafe.cdc.gov**. V-safe ni mfumo wa kufuatilia usalama ambao hukuwezesha kuielezea CDC jinsi wewe, au mtegemezi wako, unajihisi baada ya kupokea chanjo ya JYNNEOS™. Kwa taarifa zaidi tembelea **www.cdc.gov/vsafe**.

## 5. Vipi ikiwa kuna tatizo kubwa?

Athari ya mzio inaweza kutokea baada ya mtu aliyechanjwa kuondoka kwenye kliniki. Ukiona dalili za athari mbaya ya mzio (mabaka, kuvimba uso na koo, matatizo ya kupumua, moyo kudunda kwa kasi, kizunguzungu, au udhaifu), piga simu **9-1-1** na umpeleke mtu huyo kwenye hospitali iliyo karibu.

Kuhusu dalili nyingine ambazo zinakupatia wasiwasi, mpigie simu mtoa huduma wako wa afya.

Athari mbaya zinapaswa kuripotiwa kwa Mfumo wa Kuripoti Matukio Mabaya ya Chanjo (Vaccine Adverse Event Reporting System - VAERS). Mtoa huduma za afya wako kwa kawaida ataweka faili ya ripoti hii, au unaweza kufanya hivyo mwenyewe. Tembelea tovuti ya VAERS kwenye **www.vaers.hhs.gov** au piga simu **1-800-822-7967**. *VAERS ni kwa ajili ya kuripoti athari pekee, na wafanyakazi wa VAERS hawatoi ushauri wa matibabu.*

## 6. Mpango wa Hatua za Ufidiaji wa Majeraha

Mpango wa Hatua za Ufidiaji wa Majeraha (Countermeasures Injury Compensation Program) ni mpango wa serikali kuu ambao unaweza kusaidia kulipia gharama za uuguzi wa kimatibau na gharama nyingine mahususi za watu fulani ambao wamejeruhiwa vibaya sana na dawa fulani au chanjo. Ikiwa umejeruhiwa na chanjo ya ndui/monkeypox, unaweza kupata maelezo zaidi kuhusu Mpango huu kwa kutembelea tovuti ya mpango huo katika **www.hrsa.gov/cicp**, au upige simu **1-855-266-2427 (855-266-CICP)**.

## 7. Ninaweza kupataje maelezo zaidi?

- Muulize mtoa huduma za afya wako.
- Piga simu kwenye idara ya afya eneo lako au ya jimbo.
- Tembelea tovuti ya Shirika la Chakula na Dawa (Food and Drug Administration - FDA) upate machapisho ya vifurushi vya chanjo na taarifa ya ziada katika **www.fda.gov/vaccines-blood-biologics/vaccines**.
- Wasiliana na Vituo vya Kudhibiti na Kuzuia Magonjwa (Centers for Disease Control and Prevention - CDC):
  - Piga simu **1-800-232-4636 (1-800-CDC-INFO)** au
  - Tembelea tovuti ya CDC katika **www.cdc.gov/poxvirus/monkeypox**.

**Swahili** translation provided by Immunize.org